# WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI



## JARIDA MAALUM
# MBEYA

# UTAMBUZI WA VIPANDE VYA ARDHI


BODI YA UHARIRI

**MARY MAKONDO**
Mwenyekiti

**LUSAJO MWAKABUKU**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAANDISHI**
Munir Shemweta
Eliafile Solla
Hassan Mabuye
Magreth Lyimo



Mji wa Serikali Mtumba, S. L. P. 2908 | 40477- DODOMA | Simu: +255 262 963309/13/14 | Nukushi: +255 262 963316
Barua pepe: ps@lands.go.tz | Tovuti: www.lands.go.tz



*Mratibu wa zoezi la Utambuzi kila kipande cha Ardhi katika mkoa wa Mbeya ambaye pia ni Mpima wa mkoa Leosi Mwenda akizungumza na wananchi wa kata ya Sinde katika halmashauri ya jiji la Mbeya wakati wa kutambulisha zaoezi hilo mwishoni mwa wiki.*

# WIZARA YA ARDHI KUTAMBUA VIPANDE VYA ARDHI KATIKA MITAA 32 MBEYA

**Na Munir Shemweta**

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeanza zoezi la kutambua vipande 17,000 vya ardhi katika kata sita zenye mitaa 32 katika halmashauri ya jiji la Mbeya.

Hatua hiyo ni jitihada za Wizara ya Ardhi kuhakikisha inatambua maeneo yote yaliyojengwa kiholela nchini ambapo katika kata hizo Wizara imetoa jumla ya Shilingi milioni 145 kwa ajili ya kuendesha zoezi hilo.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Sinde katika halmashauri ya jiji la Mbeya mwishoni mwa wiki Mratibu wa zoezi hilo ambaye ni Mpima wa mkoa wa Mbeya Leosi Mwenda alisema kuwa, kwa sasa zoezi hilo limeanza kwenye kata mbili za Sinde na Ilemi zenye jumla ya mitaa kumi na mbili.

*''Hivi sasa vijana wapo kazini katika Kata mbili kwa ajili ya utambuzi wa vipande vya ardhi na katika zoezi hilo vijana wanatumia simu janja katika kufanikisha zoezi hilo na mfumo wenyewe wa utambuzi utasomeka Wizarani''* alisema Mwenda.

Kwa mujibu wa Mratibu huyo, kabla ya kuanza zoezi hilo timu yake ilikutana na viongozi wa maeneo yanayopitiwa na zoezi hilo wakiwemo madiwani, watendaji na wenyeviti wa mitaa pamoja na mabalozi kuwapatia semina elekezi kwa nia ya kuwajengea ufahamu wa zoezi hilo.

Mwenda alisema, Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa linakofanyika zoezi wamefanya kazi kubwa ya kuwafahamisha wananchi kuhusiana na zoezi hilo na kuwafanya kulipokea vizuri na hivyo kufanya kazi kuwa nyepesi.

Alizititaja kata zitakazofikiwa na zoezi hilo la utambuzi katika halmashauri ya jiji la Mbeya kuwa ni kata za Ilemi, Isanga, Sinde, Meanga, Mabatini pamoja na Nzovu ambazo zote kwa pamoja zina jumla ya mitaa 32.

Kwa upande wake Afisa Ardhi Mteule wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya Advent Tweve alisema, kazi kubwa ya zoezi hilo ni kufanya utambuzi wa vipande vya ardhi katika makazi holela na kuwapatia wamiliki wake leseni za Makazi ambapo alieleza kuwa, kabla ya kuanza zoezi hilo kuliundwa kamati za wananchi kwenye mitaa kwa lengo la kutatua changamoto na kutoa taarifa sahihi kwa wamiliki katika mitaa husika.

Kwa mujibu wa Tweve, leseni za makazi zitakazotolewa ni nyaraka kama zilivyo nyaraka nyingine za ardhi ingawa hizo hutolewa katika maeneo yasiyopangwa na kupimwa na gharama yake ni ndogo.

# WANANCHI WAELEZWA AINA ZA UMILIKI ARDHI KATIKA ZOEZI LA UTAMBUZI MAKAZI HOLELA

Na Munir Shemweta

Imeelezwa kuwa, wakati wa zoezi la utambuzi kila kipande cha ardhi katika makazi holela kwenye kata sita zenye mitaa 32 katika halmashauri ya jiji la Mbeya, kila mmiliki wa ardhi ataulizwa aina ya umiliki anaotaka kutambuliwe wakati wa zoezi hilo.

Akizungumza na wananchi wakati wa zoezi hilo katika kata ya Sinde halmashauri ya jiji la Mbeya hivi karibuni, Mratibu wa zoezi hilo ambalo wamiliki watapatiwa Leseni za Makazi Leosi Mwenda alisema, wataalamu wanaoendesha zoezi hilo watakapofika kwa wamiliki wa wahusika wataulizwa aina ya umiliki wanaotaka uwepo kwenye nyaraka.

Ametaja umiliki unaotambuliwa kuwa, ni umiliki wa pekee alioueleza kuwa mhusika hatakuwa na ushirika na mtu mwingine yeyote, umiliki wa pamoja usio gawanyika na kuhusisha mume na mke alioulezea kuwa wahusika wote wawili watapiga picha zitakazowekwa kwenye nyaraka na ikitokea mmoja kati yao kafariki basi aliyebaki atabaki kuwa mmiliki halali.

Kwa mujibu wa mratibu huyo wa zoezi la utambuzi vipande vya ardhi mkoa wa Mbeya, umiliki mwingine ni ule ulio chini ya Mirathi ambao utaonesha mhusika anamiliki chini ya usimamizi wa mirathi na majina ya wanufaika yataainishwa.

Aidha, umiliki mwingine ni ule wa chini ya Mlezi ambapo Mwenda alisema sheria ya ardhi hairuhusu mtoto chini ya miaka 18 kumiliki ardhi hivyo mtoto husika atakapovuka miaka 18 ndiyo atakuwa mmiliki halali wa ardhi. Pia aliitaja aina nyingine ya umiliki kuwa ni umiliki chini ya hisa utakaohusisha mtu zaidi ya mmoja.

Alifafanua kuwa, katika umiliki huo wamiliki wanaweza kuwa walinunua eneo pamoja na ikitokea wa mmoja wa wamiliki wa hisa amefariki basi familia yake itanufaika.

Mwenda alisema, umiliki wa mwisho ni wa Taasisi alioueleza kuwa majina yatakayoonekana kwenye nyaraka ni yale ya bodi ya wadhamini na kusisitiza kuwa leseni za makazi katika zoezi hilo zitazingatia miliki zote zilizoainishwa huko nyuma.



*Diwani wa Kata ya Sinde katika halmashauri ya jiji la Mbeya Fanuel Kyanula akizungumza na wananchi wa kata ya Sinde katika halmashauri ya jiji la Mbeya wakati wa kutambulisha zaoezi la kutambua kila kipande cha ardhi katika kata hiyo hilo mwishoni mwa wiki.*

# MBEYA WAELEZWA FAIDA ZA LESENI ZA MAKAZI

**Na Munir Shemweta**

Afisa Ardhi Mteule wa halmashauri ya jiji la Mbeya Advent Tweve amesema, zoezi la utambuzi kila kipande cha ardhi kwa wamiliki wanaoishi kwenye makazi holela Jijini Mbeya lina faida kubwa ikiwemo kuepuka taarifa za udanganyifu na ubadilishaji mipaka kutoka kwa baadhi ya wamiliki wa ardhi.

Aidha, alisema utambuzi huo utasaidia pia ardhi kutambulika kisheria na nyaraka zake kutumika mahakamani kama ushahidi.

Akielezea zaidi faida za zoezi la utambuzi kila kipande cha ardhi katika halmashauri ya jiji la Mwanza, Tweve alizitaja faida nyingine kuwa, ni pale inapotokea suala la fidia mmiliki atakuwa anakubalika kisheria kwa kuwa ana nyaraka na malipo kuhusiana na fidia yatategemea makubaliano baina ya mmiliki na yule anayetaka kulipa fidia.

Faida nyingine kwa mujibu wa Afisa Ardhi Mteule katika halmashauri ya jiji la Mbeya, ni mmiliki kutumia nyaraka za umiliki kuchukua mikopo Benki, kumdhamini mtuhumiwa mahakamani, kuondoa migogoro ya mipaka kwa kuwa taarifa za wamiliki ziko kwenye kanzidata na kuonesha uhalisia wa mipaka pamoja na thamani ya ardhi kuongezeka.

"Ukiwa na nyaraka za umiliki thamani ya ardhi yako inaongezeka maana madalali wakitaka kuuza kiwanja chako watauliza kina hati? Maana yake wanataka kujua ardhi yako iko salama na haina mashaka?" Alisema Tweve.

Alieleza kuwa, ni muhimu wamiliki wa ardhi zilizo kwenye makazi holela wakachangamkia zoezi hilo kwa kupima maeneo yao na kusisitiza suala la kodi ya ardhi lisiwatishe kwa kuwa siyo kandamizi na gharama yake ni ndogo ambapo mita moja ya mraba ni shilingi 32.

*"Gharama ya kodi wala siyo kubwa kama eneo lako ni mita za mraba 100 hapo utazidisha kwa 32 unapata 3200 hiyo ndiyo kodi yako kwa mwaka ila usiilimbikize na ukilipa kwa wakati haina shida tofauti kabisa na kodi ya jengo"* alibainisha Tweve.



*Afisa Ardhi Mteule wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya Advent Tweve akizungumza mbele ya wananchi wa kata ya Sinde wakati wa kutambulisha zaoezi la kutambua kila kipande cha ardhi katika kata hiyo hilo mwishoni mwa wiki.*



Sehemu ya wananchi wa kata ya Sinde katika halmashauri ya jiji la Mbeya wakifuatilia maelezo yanayotolewa wakati wa kutambulisha zoezi la kutambua kila kipande cha ardhi katika kata hiyo hilo mwishoni mwa wiki.



# CHANGAMKIENI ZOEZI LA LESENI ZA MAKAZI

## Na Munir Shemweta

Diwani wa kata ya Sinde katika halmashauri ya jiji la Mbeya Fanuel Kyanula amewataka wananchi wa kata yake kuchangamkia zoezi la utambuzi maeneo ya makazi holela ili waweze kupatia leseni za Makazi.

Akizungumza na wakazi wa kata ya Sinde wakati wa kutambulisha zoezi hilo hivi karibuni jijini Mbeya Kyanula alisema, zoezi hilo sasa linawapa uhakika wananchi wake kwa kuwa muda mrefu wameshindwa kufanya maendelezo katika maeneo yao kwa hofu ya kutokuwa na uhakika wa miliki.

" Jambo hili sasa linatoa uhakika na miaka yote mmeshindwa kuendeleza vibanda lakini sasa limetokea na mnatakiwa kutoa 10,000 tu, ningependa zoezi lifanyike haraka katika kata hii ya Sinde" alisema Kyanula.

Diwani huyo wa kata ya Sinde alieleza kuwa, kabla ya kuanza zoezi la utambuzi aliona aanze na mikutano na wananchi ili wawe na amani na zoezi hilo na kubainisha kuwa haina maana akina mama wa kata yake wapate shida ya mikopo kutokana na kukosa nyaraka za umiliki ardhi.

*" Wana Sinde siyo muende kukopa kwa vishoka asilimia 40 kwa 60 na mtakapopata leseni za makazi kupitia zoezi hili mtaweza kukopa katika taasisi za fedha hivyo changamkieni" alisema.*

Aliwatahadharisha wananchi wa kata yake kuwa, ili zoezi hilo liende vizuri lazima ziundwe kamati za uhakika na kubainisha kuwa kazi ya kamati hizo ni kutatua migogoro midogomidgo kwenye mitaa kabla ya zoezi la utambuzi kuanza na kutaka kazi hiyo kufanyika kwa haraka.

# UTAMBUZI MAKAZI HOLELA MBEYA WAWAKUNA WANANCHI

**Na Munir Shemweta**



Baadhi ya wananchi katika kata ya Sinde halmashauri ya jiji la Mbeya mkoani Mbeya wamefurahishwa na zoezi la utambuzi makazi holela linalofanyika kwenye mitaa yao na kueleza kuwa zoezi hilo linawafanya kuwa na umiliki halali wa maeneo yao.

Walisema, zoezi hilo walisubiri kwa muda mrefu kwa kuwa lilikuwa kwenye mpango wa maendeleo mijini na vijijini tangu miaka ya tisini lakini lilichelewa na utekelezaji wake sasa unawapa faraja katika kumiliki ardhi.

*" Zoezi hili limechelewa sana na tumelisubiri kwa muda mrefu na sijaona sababu ya kuchelewa" alisema Ambonise Mwaiselo mkazi wa kata ya Sinde*

Baadhi ya wananchi wa kata ya Sinde waliuliza maswali mbalimbali kwa lengo la kupata ufahamu zaidi wa zoezi hilo la utambuzi makazi holela.

Miongoni mwa maswali hayo ni, namna ya kumiliki ardhi kupitia leseni za makazi, upatikanaji barabara katika maeneo yanyofanyiwa utambuzi, umiliki wa pamoja baina ya mume na mke, tofauti ya leseni za makazi na hatimiliki ya ardhi, tofauti ya kodi ya

Mtendaji wa mtaa wa Mapelele katika halmashauri ya jiji la Mbeya Dias Mwaipape alieleza kuwa, muitikio wa wananchi katika mtaa wake ni mzuri na wanaonesha ushirikiano wa hali ya juu kuhusiana na zoezi hilo.

Zoezi la utambuzi makazi holela mkoani Mbeya unafanyika katika kata sita zenye mitaa 32 ambapo jumla ya vipande vya ardhi 17,000 vitafikiwa na kupatiwa leseni za makazi.



*Mmoja wa vijana wanaoendesha zoezi la utambuzi wa vipande vya ardhi katika mtaa wa Makerere Assah Mwakobela (kushoto) akichukua taarifa za umiliki wa ardhi kwa Bi. Elisia Kwai (wa pili kulia) wakati wa zaoezi la kutambua kila kipande cha ardhi katika kata hiyo hilo mwishoni mwa wiki.*